JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS

TAASISI YA UONGOZI

UONGOZI Institute

# TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

## TAASISI YA UONGOZI KUFANYA MAHAFALI YA NANE

**16 Mei 2025, Dar es Salaam:** Sherehe ya mahafali ya nane ya Taasisi UONGOZI itafanyika leo katika Ukumbi wa Mikutano wa Mlimani City, Jijini Dar es Salaam. Mgeni Rasmi wa Tukio hili atakuwa Mhe. George Boniface Simbachawene (Mb) Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Wasilisho kuu litatolewa na Bibi Suzanne Innes-Stubb, Mke wa Rais wa Finland na mtaalamu mwandamizi wa kimataifa katika masuala ya sheria na maadili.

Tukio hili linafanyika kwa ajili ya kuwapongeza viongozi waliomaliza programu za mafunzo ya muda mrefu: Stashahada ya Uzamili ya Uongozi (*Postgraduate Diploma in Leadership*), Programu ya Uongozi Ngazi ya Cheti (*Certificate in Leadership*), na Programu ya Uongozi kwa Wanawake (*Women's Leadership Programme*). Wageni watakaohudhuria ni pamoja na viongozi waandamizi kutoka nchi mbalimbali barani Afrika – na sekta zote ikiwemo sekta ya umma, sekta binafsi, sekta ya elimu ya juu, na sekta ya asasi za kiraia. Jumla ya viongozi 200 watahitimu.

Lengo la programu hizi ni kujenga na kuimarisha uwezo wa viongozi katika maeneo matatu: sifa binafsi za uongozi, usimamizi wa rasilimali watu, na uongozi wa taasisi. Zimeandaliwa kwa ajili ya viongozi wanaotaka kujiendeleza bila kukwamisha kazi yao. Wakufunzi wa programu ni wataalamu wabobezi katika masuala ya uongozi kutoka nchi mbalimbali duniani.

Stashahada ya Uzamili ya Uongozi na Programu ya Uongozi Ngazi ya Cheti zimeandaliwa na kutolewa kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Aalto cha Mafunzo ya Utawala, kilichopo nchini Finland. Utekelezaji wa programu hizi mbili unawezeshwa kwa kiasi kikubwa na Serikali ya Tanzania na Serikali ya Finland. Programu ya Uongozi kwa Wanawake inafadhiliwa na Serikali hizo mbili pamoja na Umoja wa Ulaya, na Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia masuala ya wanawake (UN Women).

Ushiriki katika tukio hili ni kwa mwaliko pekee.

Imetolewa na,

Suzana Aroko

**Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano kwa Umma**

Kiwanja Na. 100, 1 Barabara ya Magogoni, Kivukoni. S.L.P. 105753, 11101 Dar es Salaam. Simu: +255 22 211 0372/3. Nukushi: +255 22 211 0374. Barua pepe: barua@uongozi.go.tz. Tovuti: www.uongozi.go.tz.